Jarida Maalum
HALMASHAURI YA
JIJI LA DODOMA
TOLEO NA. 015

# Ziara ya Kamati ya Fedha na Utawala Robo ya kwanza 2024/25






MIRADI

UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA
JIANDIKISHE PIGA KURA
2024
OFISI YA RAIS TAMISEMI

JIJI LA DODOMA

# MRADI WA JENGO SHULE YA SEKONDARI MKONZE







Mradi wa utekelezaji wa vyumba sita vya madarasa na matundu nane ya vyoo Shule ya Sekondari Mkonze unagharimu kiasi cha shilingi 152,400,000.00 Fedha kutoka Serikali kuu.

Mradi ulianza Juni, 2024 na kukamilika tarehe 30 Septemba, 2024.

Kukamilika kwa ujenzi wa mradi huo kutatatua changamoto ya miundombinu ya vyoo na madarasa inayoikabili shule ya sekondari Mkonze kutokana na ongezeko la wanafunzi mwaka hadi mwaka ambapo kwasasa shule inajumla ya wanafunzi 1268.

# MRADI WA ZAHANATI YA MSEMBETA






Kamati ya Fedha na Utawala imekagua utekelezaji wa mradi wa zahanati ya Msembeta, iliyopo kata ya Chigongwe. Mradi umegharimu kiasi cha shilingi 181,000,000.00 ambazo kati ya hizo shilingi 150,000,000.00 fedha kutoka Serikali kuu, shilingi 65,000,000.00 fedha kutoka Mapato ya ndani ya halmashauri na shilingi 16,000,000.00 ni nguvu ya wananchi na wadau wa maendeleo.

Kukamilika kwa mradi huo kutawasaidia wananchi wa Mtaa wa Msembeta na maeneo jirani kupata huduma za afya karibu na maeneo wanayoishi.

Mradi wa zahanati ya Msembeta ulianza kutekelezwa Mei, 2018 kupitia michango, nguvu za wananchi na wadau wa maendeleo ambapo kiasi cha shilingi 16,000,000.00 kilipatikana na kuanza kutekeleza hatua za awali za ujenzi wa mradi huo.

# KAMATI YA FEDHA YATEMBELEA AGAPE WOMEN GROUP



Halmashauri ya Jiji la Dodoma ilikiwezesha Kikundi cha Agape Women mkopo usio na riba wa asilimia nne kutoka mapato ya ndani kiasi cha shilingi 50,000,000.00 kwa lengo la kukuza mtaji wa biashara ya ushonaji wa nguo. Katika fedha hiyo, kiasi cha shilingi 26,000,000 kimerejeshwa.

Lengo la Kikundi cha Agape Women ni kutumia fursa ya ushonaji kujiajiri, kuongeza kipato na kujikwamua kiuchumi.

Ikumbukwe kuwa Kikundi cha Agape Women ni mkopo wake w a tatu, awamu ya kwanza kilikopeshwa shilingi 7,000,000 na awamu ya pili kilikopeshwa shilingi 15,000,000.00.

# VITUO VYA AFYA

**MIRADI YA UFADHILI WA SERIKALI KUU**

**MIRADI YA MAPATO YA NDANI**



## UJENZI WA KITUO CHA AFYA CHIGONGWE

**Mradi umekamilika na huduma zinaendelea**

# UJENZI WA BWENI HOMBOLO MAKULU

*FEDHA KUTOKA SERIKALI KUU*







## UJENZI WA BWENI LA WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUM

Kamati ya Fedha na Utawala imekagua mradi wa Bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalum shule ya msingi Hombolo Bwawani. Mradi unagharimu kiasi cha shilingi 150,000,000.00 ambapo shilingi 100,000,000.00 ni fedha kutoka Serikali kuu na shilingi 50,000,000.00 ni fedha za Mapato ya ndani ya halmashauri.

Shule ya msingi Hombolo Bwawani ilianza mwaka 1961 ina jumla ya wanafunzi 1290 kati yao wavulana ni 637 na wasichana ni 653 kati ya wanafunzi hao wenye mahitaji maalum ni 78 (wavulana 48 na wasichana 30).

“ Tunaupongeza uongozi wa shule na kata kwa kazi nzuri hili Bweni ni muhimu kwa watoto wetu sisi kama kamati tunamuagiza mkurugenzi wa jiji ahakikishe anatoa kiasi cha fedha kilichobaki kwaajili ya umaliziaji wa mradi” Diwani Daud Mkhandi.

# MRADI WA UJENZI WA OFISI YA CHAHWA

*FEDHA KUTOKA SERIKALI KUU*



**MUONEKANO WA JENGO LA OFISI YA KATA CHAHWA**





Mradi wa ujenzi wa ofisi ya kata Chahwa ulianzishwa kwa nguvu za wananchi wakishirikiana na Diwani Mheshimiwa, Sospeter Mazengo mwaka 2019.

Disemba 2019 Ofisi ya Mkurugenzi ilitoa kiasi cha shilingi 10,000,000.00 kuunga mkono juhudi za wananchi, kati ya fedha hizo shilingi 4,000,000.00 ilitumika kununua kiwanja na Tsh. 6,000,000 ilitumika kuanzisha ujenzi kwa ununuzi wa tofali na saruji.

Mpaka sasa mradi umegharimu kiasi cha shilingi 45,000,000.00 kwa mchanganuo ufuatao; shilingi milioni 15,000,000.00 fedha kutoka mapato ya ndani ya halmashauri na shilingi 30,000,000.00 fedha iliyotokana na fidia ya kupisha upanuzi wa Ikulu ya Chamwino.

# MRADI WA UJENZI WA OFISI YA KATA IPAGALA

MAPATO YA NDANI



## MUONEKANO WA UJENZI WA JENGO LA OFISI YA KATA IPAGALA

Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Kata Ipagala ulianza kutekelezwa Agosti, 2023 ukihusisha unyanyuaji wa kuta , kumwaga lenta, kupaua, kujenga matungulizi, kufanya brandeling na kuchimbia miundombinu ya maji na umeme.

Mpaka sasa mradi umegharimu kiasi cha shilingi 27,45,000.00 ikiwa ni gharama ya vifaa na malipo ya fundi.





# KAMATI YA FEDHA YATEMBELEA KIKUNDI CHA BODABODA

*MAPATO YA NDANI*








## KAMATI YA FEDHA NA UTAWALA ROBO YA KWANZA NA KIKUNDI CHA BODABODA

Kikundi cha vijana JERAK ni kikundi kinachojishughulisha na shughuli za usafirishaji kwa kutumia bodaboda na bajaji katika kituo cha Golden Folk jijini Dodoma.

Ni moja kati ya kikundi nufaika na mkopo wa asilimia nne wa vijana usio na riba unaotelewa na halmashauri. Kikundi cha JERAK kilikopeshwa kiasi cha shilingi 17,000,000.00, mpaka sasa kikundi kimefanikiwa kumaliza deni kwa kurejesha kiasi cha shilingi 17,000,000.00.

“Ninawapongeza kwa kumaliza marejesho ndani ya mwaka mmoja badala ya miwili,niwaombe muendelee kujipanga zaidi kwa kuongeza vyombo vya usafiri kama bajaji na guta” alisema Diwani Beatrice Ngerangera.

# MIRADI YA ELIMU



MIRADI YA UFADHILI WA SERIKALI KUU

MIRADI YA MAPATO YA NDANI

**UJENZI WA SHULE YA SEKONDARI HOMBOLO MAKULU**

**UJENZI WA MADARASA YA MFANO SHULE YA MSINGI MICHESE**

# PICHA ZA MIRADI MBALIMBALI YA ELIMU








# UJENZI WA MRADI WA SHULE YA MPUNGUZI SEKONDARI

## FEDHA KUTOKA SERIKALI KUU



Mradi unatekelezwa katika Kata ya Mpunguzi eneo la Mpunguzi sekondari.

Gharama ya mradi ni Shilingi 83,400,000.00 fedha kutoka Serikali Kuu.

Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 95 huku kazi iliyosalia ni ufungaji wa swichi za taa na umeme.
kukamilika kwa mradi huu kutaboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwa wanafunzi na walimu.

"Kazi nzuri sana imefanyika tunaagiza usimamizi uendelee kwa kazi zilizobakia ili zikamilike kwa wakati na watoto wetu waanze kunufaika na mradi" Diwani Awadh Abdallah.





# MRADI WA UJENZI WA MADARASA SHULE YA SEKONDARI MTEMI CHILOLOMA

*FEDHA KUTOKA SERIKALI KUU*



Mradi unagharimu kiasi cha shilingi 140,000,000.00 fedha kutoka Serikali kuu ukihusisha Ujenzi wa madarasa sita.

Mradi ulianza kutekelezwa Juni, 2024 unatarajia kukamilika tarehe 30 Oktoba, 2024. Mpaka sasa utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 90 ambapo kazi zilizobaki ni ukamilishaji wa kuweka marumaru, rangi, madirisha na milango.





# MRADI WA UJENZI WA MADARASA MAWILI NA MATUNDU NANE YA VYOO KATIKA YA SHULE YA SEKONDARI IPALA

*FEDHA KUTOKA SERIKALI KUU*



Mradi unatekelezwa Kata ya Ipala ukigharimu kiasi cha Shilingi 60,400,508.90 fedha kutoka Serikali kuu.

Kazi zilizotekelezwa ni upauaji wa madarasa mawili, brandering, uchimbaji na ujenzi wa mashimo ya vyoo pasipo kufunika na upauaji wa matundu nane ya vyoo.

Kiasi kilichotumika ni shilingi 34,233,750 na kiasi kilichobaki ni shilingi 26,166,758.90. Mradi ulianza Julai, 2024 unatarajiwa kukamilika tarehe 03, Novemba, 2024





# MRADI WA UJENZI WA MATUNDU 08 YA VYOO NA MADARASA 03 MBALAWALA SEKONDARI

*FEDHA KUTOKA SERIKALI KUU*



Halmashauri ya Jiji la Dodoma kupitia mapato yake ya ndani ilitoa kiasi cha shilingi 83,400,000.00 kwaajili ya ujenzi wa matundu 18 ya vyoo, darasa moja na umaliziaji wa madarasa matatu na ofisi moja shule ya sekondari Mbalawala.

Ujenzi upo hatua ya umaliziaji.







# MRADI WA UJENZI WA SHULE YA ITEGA SEKONDARI


*FEDHA KUTOKA SEQUIP*



Kamati ya Fedha na Utawala imekagua ujenzi wa madarasa matatu na matundu nane ya vyoo shule ya sekondari Itega.

Mradi unagharimu kiasi cha shilingi 84,400,000.00 fedha kutoka Serikali kuu kupitia mradi wa SEQUIP.

Ujenzi wa mradi umekamilika kwa asilimia mia ikiwa ni pamoja na samani zake.





# UJENZI WA MADARASA YA MFANO SHULE YA MSINGI MACHESE

*FEDHA KUTOKA MRADI WA BOOST*



Fedha zilizopelekwa: shilingi 65,600,000.00

Chanzo cha fedha : Serikali kuu kupitia mradi wa Boost.

Mradi unahusisha ujenzi wa madarasa mawili ya awali na matundu sita ya vyoo





# MRADI WA UJENZI WA VYUMBA VIWILI VYA MADARASA NA MATUNDU NANE YA VYOO SHULE YA SEKONDARI ZUZU

*FEDHA KUTOKA SERIKALI KUU*



Fedha zilizopokelewa: Shilingi 60,400,000.00

Chanzo cha fedha: Serikali kuu

Fedha zilizotumika: Shilingi 60,200,000.00

Utekelezaji: Ujenzi umekamilika kwa asilimia 100





# MRADI WA UJENZI WA DARASA 1 NA MATUNDU 08 YA VYOO SHULE YA SEKONDARI MBABALA

*FEDHA KUTOKA SERIKALI KUU*




Fedha zilizopokelewa: Shilingi 37,400,000.00

Fedha zilizotumika: Shilingi 28,632,450.00

Fedha zilizobaki: Shilingi 8,767,550.00

Chanzo cha fedha:  Serikali kuu

Ujenzi upo hatua ya umaliziaji bado plasta, skim, vigae, rangi, madirisha na milango. upande wa ujenzi wa matundu ya vyoo shimo limechibwa na kujengwa bado kufunikwa.





# MRADI WA UJENZI WA VYUMBA VITATU VYA MADARASA NA MATUNDU NANE YA VYOO SHULE YA SEKONDARI MNADANI

*FEDHA KUTOKA SERIKALI KUU*



Lengo la mradi : Ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa na matundu nane ya vyoo katika Shule ya Sekondari Mnadani umelenga kuondoa msongamano wa wanafunzi katika madarasa.



Gharama za mradi: Shilingi 83,400,000.00

Chanzo: Fedha kutoka Serikali kuu

Hatua ya utekelezaji: Mradi umekamilika hatua zote kwa ujenzi wa madarasa isipokuwa matundu nane ya vyoo yapo katika hatua ya kupaua.



Jarida Maalum
HALMASHAURI YA
JIJI LA DODOMA
TOLEO NA. 015

# Ziara ya Kamati ya Fedha na Utawala Robo ya kwanza 2024/25

JIJI LA DODOMA

JARIDA HILI LINATOLEWA NA
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA
**S.L.P 1249 DODOMA, TANZANIA**
**Baruapepe: cd@dodomacc.go.tz**
**Tovuti: www.dodomacc.go.tz**